

# MAMLAKA YA MAJI SAFI NA MAJI TAKA MJINI MOSHI



## WIZI WA HUDUMA

Utafiti wa muda mrefu uliofanywa na Mamlaka umethibitisha kuwa baadhi ya Wateja ama Nyumba ambazo si za Wateja wa Mamlaka zimekuwa na tabia mbaya ya **Wizi wa Huduma ya Maji Safi na Maji Taka** kwa kujiunganishia wenyewe.

Kulingana na Sheria za Maji Nchini za Mwaka 1974, 1999 na CAP 281 ni Kosa la Jinai Kujiunganishia Huduma ya Maji Safi na Maji Taka Bila ya Idhini ya Mamlaka za Maji Safi na Maji Taka Nchini zinazohusika.

Sheria ya Maji imeipa Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mjini Moshi uwezo wa;

- Kufanya Ukaguzi katika Nyumba ama Eneo la Mteja wakati wowote iwapo Eneo ama Nyumba husika itahisiwa kuwa na wizi, uvujaji ama upotevu wowote wa rasilimali ya maji.

Mamlaka inapenda kuwataarifu Wakazi wote wa Mji wa Moshi kuwa ni Kosa kwa Mteja ama Mmiliki yeyote wa Nyumba katika Mji wa Moshi kuwazuia Wataalamu na Mafundi wa Mamlaka kufanya Ukaguzi katika Nyumba ama Eneo lake kuhusiana na Huduma ya Maji Safi na Maji Taka.

---

Iwapo Mteja ama Nyumba ya Mkazi yeyote wa Mji wa Moshi atakutwa na Wizi wa Maji, Mamlaka italazimika kufuata utaratibu ufuatao:

- Kung'oa Mtandao (Bomba) za Maji Safi na Maji Taka zilizounganishwa
- Kukatisha Huduma ya Maji Safi na Maji Taka kwa Mhusika.
- Kutumia sheria ikiwa ni pamoja na Kumshitaki Mhusika, Kudai Fidia ya matumizi ya maji kulingana na muda aliotumia huduma na Fidia ya Usumbufu ambayo ni Tshs. 150,000/= kwa Wateja wa Majumbani na Tshs 250,000/- kwa Wateja wa Biashara, Taasisi na Viwanda.

Jihadhari na Mafundi wa Mtaani ni **HATARI** kwani hawana Leseni wala Kibali cha Kukuunganisha katika Huduma ya Maji Safi na Maji Taka katika Mji wa Moshi. Ni Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mjini Moshi pekee yenye uwezo Kisheria wa Kukuunganishia Huduma hizi muhimu.

Unapokutana na Mafundi Walaghai wa Mtaani, tafadhali wadadisi na uwaulize kama wanacho Kitambulisho na Kibali cha Mamlaka kufanya kazi hiyo.

Wasiliana na Kitengo cha Mahusiano na Wateja (Huduma kwa Wateja) ili kupata Maelezo kuhusu Utaratibu wa Kuunganishwa katika Huduma ya Maji Safi na Maji Taka.

**MKURUGENZI MTENDAJI**  
**MAMLAKA YA MAJI SAFI NA MAJI TAKA**  
**MJINI MOSHI**  
S.L.P 324, MOSHI Simu: 2751164  
Barua Pepe: [muwasa@kilionline.com](mailto:muwasa@kilionline.com)

---